**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA**

SHULE YA SEKONDARI LANG'ATA BORA,
S.L.P. 208,
MWANGA
Tarehe……………

Kumb. Na. LBSS/JI/VOL.I/……………

KWA MZAZI/MLEZI WA ………………………………………………………………………….

S.L.P……………………………….

……………………………………………….

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI LANG'ATA BORA, WILAYA YA MWANGA, MKOA WA KILIMANJARO MWAKA 2021.**

## 1.0 UTANGULIZI

Nafurahi kukuarifu kwamba mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari Lang'ata bora ipo kata ya Lang'ata kando ya bwawa la Nyumba ya Mungu umbali wa km 23 kutoka makao makuu ya Wilaya ya Mwanga. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 11/01/2020. Anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 11/01/2021 saa 1.00 asubuhi na mwisho wa kuripoti ni tarehe 18/01/2021

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1 SARE ZA SHULE

1) Shati mbili (2) nyeupe za mikono mifupi (tetron)
2) Suruali mbili (2) za khaki kwa wavulana na sketi mbili (2) za khaki kwa wasichana. Sketi ziwe na urefu usiopungua inchi 9 kwenda chini kuanzia kwenye magoti. Suruali za kubana hazitaruhusiwa upana wa suruali usipungue sentimeta 17 au inchi 7(Kitambaa cha suruali na sketi kimeambatanishwa na fomu hii).
3) Viatu vyeusi vya kamba vyenye visigino vifupi.
4) Soksi jozi mbili (2) nyeupe kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana.

5) Sweta ya rangi ya khaki inayofanana na rangi ya sketi / suruali.
6) T- shirt yenye nembo ya shule, rangi itakayochaguliwa utaelekezwa baada ya kuripoti shuleni.
7) Sare za michezo ni *track suit* ya bluu na fulana ya bluu pamoja na bukta ya bluu kwa wavulana. Wasichana ni *track suit* ya bluu na fulana ya bluu.
8) Raba rangi yoyote

2.2 (i) Madaftari makubwa 10 (counter books) za three quire.
(ii) Kalamu za wino na penseli za kutosha
(iii) Mathematical set (mkebe wa vifaa vya Hisabati)
(iv) Wanafunzi wa kutwa walete ndoo ndogo mpya kwa ajili ya matumizi ya shule.

2.3 Chakula cha mchana kwa wanafunzi wa kutwa ni wajibu wa mzazi/mlezi kuhakikisha mwanafunzi anapata chakula cha mchana shuleni.

**3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa na sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo inayotolewa na Wizara Elimu na Mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambapo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi,wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumala ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
(d) Kuwahi katika kila shuguli za shule na nyingine utakazopewa.
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote, na
(i) Kutunza mali ya umma.

3.1. **MAMBO YAFUATAYO YANAWEZA KUKUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE AU KUSIMAMISHWA SHULE**


a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi, matumizi ya dawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi, kuberi na sigara.
e) Kupigana au kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
g) Kudharau bendera ya Taifa
h) Kuwa mjamzito / kupata mimba
i) Kuoa au kuolewa
j) Kutoa mimba
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule na watu
l) Kuwa na simu ya mkononi

**4.0. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI**

a) *Medical Examination form* ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakapo ripoti Shuleni. Kiambatisho fomu A
b) Fomu ya mzazi / mlezi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai. Kiambatisho fomu B

**5.0. TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEZO / MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU**

**KARIBU SANA LANG'ATA BORA SEKONDARI**



**M. J. MARMO**

**MKUU WA SHULE**

**FOMU A**

**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**MWANGA DISTRICT COUNCIL**
**LANG'ATA BORA SECONDARY SCHOOL**

P.O.BOX 208
MWANGA

TO THE MEDICAL OFFICER
……………………….HOSPITAL
……………………………………….

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

Please examine……………………………………………..(Name of student) who has been selected to join this school for his/her fitness as a student in the following:-

Eyesight ……………………………………………………….
Hearing ………………………………………………………..
Speech ………………………………………………………..
Limbs ………………………………………………………….
Specimens
Urine …………………………………………………………..
Blood …………………………………………………………..
Stool ……………………………………………………………
Pregnancy …………………………………………………….
Asthma …………………………………………………………
Epilepsy ………………………………………………………..
Tuberculosis …………………………………………………...
Heart problem ………………………………………………….
Skin diseases …………………………………………………..
Any other serious diseases ………………………………………

**MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a recognized and qualified medical Doctor)
I………………………………………………….(Name of the medical Doctor)
I confirm that I have, examined ……………………..(Name of students)
And found that he/ she is physically or mentally fit/ unfit as the student.
Signature ………………………….
Designation ……………………….
Official stamp ……………………...
Date ………………………………...

This form must be filled by a recognized medical Doctor from the government hospital.



**HEAD MASTER**
**LANG'ATA BORA SECONDARY SCHOOL**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA**
**SHULE YA SEKONDARI LANG'ATA BORA S.L.P 208**

## FOMU YA KUKUBALI SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE

(Ijazwe na mwanafunzi mwenyewe kwa herufi kubwa na kisha mzazi / mlezi
Mimi______________________________________________(Jina la mwanafunzi) Naahidi kufuata sheria na taratibu zote za shule nilizoelekezwa na walimu na uongozi wa shule mara kwa mara.

Sahihi_______________________
Tarehe _________________________

**SEHEMU YA MZAZI / MLEZI**
(Sehemu hii ijazwe na mzazi/ mlezi mwenyewe)
Mimi________________________________________(jina la Mzazi/Mlezi) ninaahidi kushirikiana na waalimu na uongozi wa shule katika kuhakikisha kuwa mwanafunzi amefuata taratibu zote za shule kwa usahihi.
Pia mimi nikiwa kama mzazi / mlezi ninaahidi kutimiza mahitaji yote muhimu ya mwanangu kwa wakati ili kumpa fursa ya kupata elimu bora

Sahihi________________________

Tarehe _________________________

Anwani __________________________

Namba ya simu _____________________